



# NCHI YETU

Jarida la Mtandaoni



TOLEO NA.7

Limeandaliwa na Idara ya Habari-MAELEZO

TOLEO LA SEPTEMBER 2017

► Tanzania Yawa "Donor Country" Tiba ya Moyo Afrika ..... Uk. 13

## Reli ya Kisasa Sasa Dar-Dom



# Bodi ya Uhariri

## Mwenyekiti

Dkt. Hassan Abbasi

Mkurugenzi-Idara ya Habari-MAELEZO

## Wajumbe

Rodney Thadeus

John Lukuwi

Elias Malima

Jovina Bujulu

## Msanifu Jarida

Hassan Silayo

## Huduma zitolewazo MAELEZO

1. Kuuza picha za Viongozi wa Taifa na matukio muhimu ya Serikali.
2. Kusajili Magazeti pamoja na Majarida
3. Kukodisha ukumbi kwa ajili ya mikutano na Waandishi wa Habari.
4. Rejea ya Magazeti na Picha za Zamani
5. Kupokea kero mbalimbali za wananchi.

## Jarida hili hutolewa na:

*Idara ya Habari-MAELEZO*

*S.L.P 8031*

*Dar es Salaam-Tanzania*

*Simu : (+255) 22 -2122771*

*Barua pepe:maelezo@habari.go.tz*

*Blogu: blog.maelezo.go.tz*



**WATUMISHI HOUSING COMPANY**  
"Dhamana ya Uwekezaji katika Nyumba"



## "Hamia kwako leo"

Ikwa mkopo wa nyumba wa bei naifuu.  
Maliipo ni ndani ya mwaka 1 ili hadi miaka 25.

Kwa sasa tonajenga na kuuza nyumba bora na kisasa maeneo mbalimbali nchini:

|                               |                           |
|-------------------------------|---------------------------|
| Kigamboni (Gezaufolo)         | Mwanza (Kisesa)           |
| Morogoro (Mkundi)             | Bunju B (Mabwepande Road) |
| Magomeni (Usalama Apartments) |                           |

### PIGA SASA

0715 353 465 / 0757 437 594 / 0756 447 422



Kwa maelezo zaidi na kuweza kuchukua fomu za kununua nyumba tembelea ofisi zetu zilizopo jengo la Golden Jubilee Towers gholofa ya ilu au tembelea tovuti yetu.



@Watumishi Housing Company

[www.whctz.org](http://www.whctz.org)



## TAHARIRI

### **UAMUZI WA RAIS KUJENGA UZIO KULINDA TANZANITE UUNGWE MKONO**

Septemba 20 mwaka huu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli aliliagiza Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kujenga haraka uzio kuzunguza eneo linalochimbwa madini aina ya Tanzanite lililopo Mererani, wilayani Simanjiro Mkoa wa Manyara.

Agizo hilo lilienda sanjari na uzinduzi wa bararabara ya KIA - Mererani yenye urefu wa kilometra 26 ambayo inaunganisha eneo linalochimbwa madini la Mererani, eneo la uwekezaji la Mererani, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na barabara ya Moshi-Arusha.

Uamuzi wa kujenga uzio katika eneo la uchimbaji madini ya Tanzanite hususan kuzunguuka eneo la kitalu A mapaka D ambapo tafiti zonaonesha kuwa utajiri mwingi wa madini, una lengo la kuhakikisha rasilimali hii ya nchi inalindwa ili kuona watanzania kwa ujumla wao wanafaidika kutokana na rasilimali hiyo.

Ni jambo lililo wazi kwamba kwa muda mrefu nchi imekuwa hainufaiki ipasavyo na madini ya Tanzanite licha ya kwamba madini hayo hayapatikani sehemu nyingine yeyote zaidi ya Tanzania.

Ripoti ya hivi karibuni ya Kamati iliyoundwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Job Ndugai ilionesha kuwa Serikali na wananchi wanafaidika kwa asilimia tano fu ya madini haya adhimu huku asilimia 95 iliyobaki ikiwanufaisha watu wengine.

Kwa sababu hiyo basi, sisi NCHI YETU tunaunga mkono uamuzi wa Rais kwa asilimia mia moja uamuzi wa Rais wa kujenga uzio kuzunguuka eneo linalochimbwa madini ya Tanzanite.

Tunaamini uzio utakapojengwa kuzunguuka eneo la mgodi na kuwa na sehemu moja ambalo litatumika wakati wa kuingia na kutoka eneo la mgodi, utasaidia katika udhibiti na wizi wa Tanzanite na kuifanya biashara ya madini hayo kuwa ya uwazi.

Pia itawezesha nchi kuwa na takwimu sasa za kiwango cha madini kinachopatikana, madini hayo yameuzwa wapi na kwa thamani gani ili Taifa pia liweze kukusanya kodi na tozo stahiki zinazotokana na biashara ya Tanzanite.

Ni wazi pia kama alivyoelekeza Mhe. Rais kwamba hata soko la Tanzanite lijengwe Mererani, itaongeza thamani ya eneo hilo na kukuza uchumi wa eneo hilo kwani kwa kuibua biashara mbalimbali kutokana na wageni wengi watakaofika eneo la Mererani kwa ajili ya uchimbaji madini lakini pia kwa ajili ya utalii, kuuza na kununua madini hayo, uchumi wa eneo hilo utakuwa maradufu

Ni matumaini yetu kuwa wakazi wa Mererani na watanzania kwa ujumla watatoa ushirikiano wa kutosha kwa jeshi letu kuhakikisha nia hii njema ya Rais katika kulinda rasilimali za Taifa inafikiwa ili asilimia kubwa ya madini haya adhimu ya Tanzanite iwanufaishe wanachi walio wengi tofauti na sasa ambapo wajanja wachache wamekuwa wakifaidi neema zinazotokana na madini hayo.

# Treni ya Umeme sasa Dar-Dom

**Na. Neema Mathias- MAELEZO.**

Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli imeendelea kutekeleza Kaulimbiu yake ya Hapa Kazi Tu kwa kusaini mkataba wa pili wa ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge).

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni Hodhi ya Reli (RAHCO), Masanja Kadogosa amesaini mkataba huo mwishoni mwa mweziwatisakwaniabaya Serikali ya Tanzania na kwa upande wa mkandarasi alisaini Makamu wa Rais wa Kampuni ya Yapi Markezi Insaat Ve Senayiu kutoka Uturuki, Mr. Erdem Arioglu alisani.

Akizungumza kabla ya kusaini mkataba, Kadogosa alisema kuwa ujenzi wa reli hiyo yenye urefu wa kilometra 336 kutoka Morogoro mpaka Makutupora-Dodoma, unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi wa kumi mara baada ya kuwekwa jiwe la msingi na utakamilika katika kipindi cha miezi 36 tangu kuanza kwa ujenzi wake.

Kadogosa alieleza kuwa reli hiyo itahusisha ujenzi wa kilometra 86 za njia yakuishanira treninamaeneo ya kupangia mabehewa 422 kwa uzani wa tani 35 kwa wekeli.

Pia itahusisha ujenzi wa miundombinu ya umeme wa kuendeshea treni, ujenzi wa madaraja zaidi ya 223, makaravati zaidi ya 143, tanuru la kuitishia njia ya reli lenye urefu wa kilometra 2.5, stesheni nane za abira na njia za kupishania treni zenye urefu wa kilometra mbili.

"Kutokana na ubora wa reli hii,



**Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Profesa Makame Mbarawa akizungumza katika hafla ya utiaji saini wa mkataba wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Morogoro mpaka Makutupora, Dodoma.**

treni ya abiria itakuwa na uwezo kwenda mwendo wa kilometra 160 kwa saa wakati ile ya mizigo itakwendamwendowakilometra 120 kwa saa." alieleza bw. Kadogosa na kuongeza kuwa kutajengwa ukuta pande zote mbili za reli kuanzia Morogoro mpaka Makutupora, Dodoma na kuweka vivuko ili kuhakikisha usalama wa watu na wanyama.

Kwa upande wake Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Prof. Makame Mbarawa alisema kuwasehemuyapiliyamradihuo itagharimu Dola za Kimarekani Bilioni 1.924 na kwamba Serikali ya awamu ya tano imeupa kipaumbele mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ikiwa ni sehemu ya kuimarisha miundombinu ya usafirishaji nchini ili kuinua uchumi wa Tanzania.

"Kukamilika kwa ujenzi huo kutatoa fursa kwa viwanda na wafanyakishara kufanya chaguo la njia gani ya usafiri wenye tija watumike kusafirisha bidhaa zao. Njia hii ya reli itapunguza la gharama za usafirishaji na kuondoa hofu ya kusafirisha mizigo kwa muda mrefu kwani reli hii ya kiasasa ina uwezo wa kubeba mizigo mikubwa na inayokwenda umbalimrefunakwakasikubwa," alifanua Prof. Mbarawa.

Prof. mbarawa aliongeza kuwa usafiri wa reli una faida kubwa kwa uchumi wa nchi kwani gharama za usafirishaji zitashuka na hivyo kufanya bei za bidhaa kushuka pia kuleta nafuu katika gharama za maisha.

Mbali na kupunguza gharama



**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO) Masanja Kadogosa (kulia) na Mjumbe wa Bodii kutoka Kampuni ya Ukandarasi ya Yapi Merkezi Insaat ya nchini Uturuki wakioneshaa Mkataba wa ujenzi wa mradi wa Reli ya Kisasa kutoka Morogoro mpaka Makutopora (Dodoma).**

za usafirishaji, kukamilika kwa reli hii kutakuwa kiungo muhimu kati kati ya jiji la kibiashara la Dar es Salaam na mikoa ya kati, kanda ya ziwa mpaka nchi jirani za Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda ambazo mizigo yao mingi inapitia bandari ya Dar es Salaam.

Aidha alisema kuwa serikali kupitia bajeti ya mwaka 2016/2017 ilitenga kiasi cha shulingi Triliioni moja na katika bajeti ya mwaka 2017/2018 imetenga shilling bilioni 900 kwamba Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha kama mikopo ya bei naafuu na kuitaka kampuni hiyo kukamilishaujenzichiniiyamiezi36.

Awamu ya pili ya utajji saini ujenzi wa reli mpya ya standard gauge yenye uwezo wa kusafirisha mizigo tani million 17 kwa mwaka ni mwendelezo wa ujenzi wa awamu ya kwanza uliozinduliwa Aprili 12 wa Dar es Salaam- Morogoro wenye jumla ya kilomita 205, ikiwa ni miaka

Makutupora mpaka Tabora, ujenzi wa reli kutoka Tabora mpaka Isaka na ujenzi wa reli kutoka Isaka mpaka Mwanza.

"Kukamilika kwa ujenzi huo kutatoa fursa kwa viwanda na wafanyabiashara kufanya chaguo la njia gani ya usafiri wenye tija watumike kusafirisha bidhaa zao. Njia hii ya reli itapunguza la gharama za usafrishaji na kuondoa hofu ya kusafirisha mizigo kwa muda mrefu kwani reli hii ya kiasasa ina uwezo wa kubeba mizigo mikubwa na inayokwenda umbali mrefu na kwa kasi kubwa,"  
**alisema Prof. Makame Mbarawa**

#### DONDOD MUHIMU RELI YA KISASA MORO-DOM



# Rais Magufuli Aing'arisha Tanzania Kimataifa

**Na. Said Ameir- MAELEZO**

Mwishoni mwa mwezi Septemba tumekuwa tukisoma na wengine kuona katika vyombo vyahabari vyanidani na nje ya nchi namna Tanzania ilivyo kuwa 'gumzo' miongoni mwa wajumbe walio kuwa wakihuduria Mkutano 72 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa jijini New York nchini Marekani.

Inaelezwa kuwa nje ya kikao hicho, wajumbe walikuwa wakizungumzia zaidi uongozi wa Rais John Pombe Joseph Magufuli na mageuzi anayoyafanya ambayo, katika kipindi kifupi, yameleta matokeo chanya. Habari kutoka huko zilieleza kuwa wajumbe hao wako tayari kumualika Rais Magufuli kutembelea nchi zao ili kubadilishana uzoefu.

Tangu kuchaguliwa Dk. Magufuli kushika wadhifa wa Urais na kuanza "kutema cheche" kama aliyowahi kueleza mtangulizi wake, vyombo vyahabari vingi vya nje ikiwemo mitandao ya kijamii vimekuwa vikiwanukuu watu mbalimbali mashuhuri pamoja na wananchi wa kawaida katika nchi mbali mbali katika mabara ya Asia, Afrika na Australia wakieleza kuvutiwa na staili ya uongozi wa Rais Magufuli ya 'Hapa Kazi Tu' na kutamani viongozi wao wangefanya kama anavyofanya Dk. Magufuli.

Miezi kama mitatu iliyopita nilisoma makala moja ya mwandishi wa Sierra Leone, akielezea kukatishwa tamaa na uongozi wa nchi yake katika mapambano dhidi ya rushwa na mapungufu mengine katika Serikali yao. Mwandishi aliandika kuwa anatamani nchi yake ingepata "kiongozi kama Magufuli" na kueleza kwa kirefu hatua mbazo Rais Magufuli amekuwa akizichukua ambazo angependa rais wake nae azitekeleze.

Nilisoma pia makala moja kutoka Nigeria inayolinganisha na kupambanisha ahadi za Rais Magufuli na za Rais wa nchi hiyo huku



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akiwa na mgeni wake Mfalme wa Morocco Mohamed VI wakilakiwa na wafanyakazi pamoja na wageni mbalimbali katika viwanja vya Iklulu jijini Dar es Salaam mara baada ya kuwasili nchini kwa ziara ya kikazi.**

mwandishi akilalama kuwa kiongozi wa nchi yake ameshindwa kutimiza ahadi zake na anafaa kujifunza kutoka Rais Magufuli. Tuliwahi pia kusoma katika mitandao ya kijamii kuhusu ndoto ya baadhi ya jirani zetu kupata kiongozi kama Magufuli na wengine walipata kutunga nyimbo kusilia utendaji wake.

Kwa hiyo, Rais Magufuli kuwa 'gumzo' katika 'viunga' vya Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, mjini New York, ni mwendelezo wa sifa ambazo Rais amekuwa akizidi kujizolea kutokana na utendaji kazi wake ambao umejengeka katika kutekeleza kile anachokiamini.

Viongozi wanaoshiriki Baraza hilo hapana shaka yeyote kuwa wanamsubiri kwa hamu Rais Magufuli siku atapohuduria na kuhutubia kikao hicho kinachofanyika kila mwaka nchini humo. Hapana shaka yeyote kuwa Rais Magufuli hivi sasa sio tena 'habari ya mujini' kama wanavyosema vijana, amekuwa 'Habari ya Ulimwengu!'

Tangu ashike uongozi, Tanzania imewenza kuimarisha sana mahusiano yake na nchi washirika na wadau wa maendeleo kama mashirika ya kimataifa na ya kikanda kwa kuzingatia maudhuina malengo ya sera ya mambo ya nje ya nchi ambayo imeweka msisitizo katika diplomasia ya uchumi.

Katika kipindi hicho, Rais ametekeleza malengo hayo bila ya kufanya safari nydingi nje ya nchi na hata kufikia baadhi ya watu kuonesha wasiwasi juu ya hatua hiyo ya Mheshimiwa Rais.

Ni kweli Mheshimiwa Rais hajafanya safari nydingi za nje kama ambavyo imezooleka lakini amekuwa akifanya kazi kubwa ndani ya nchi ambayo ndio msingi wa siasa ya mambo ya nje ya nchi yeyote. Ni vyema ikumbukwe kuwa misingi ya siasa ya ndani ya nchi ndio inayoongoza siasa ya mambo ya nje ya nchi. Kwa maana nyininge, siasa ya mambo ya nje lengo lake kuu ni kujenga mazingira ya kufanikisha utekelezaji wa malengo ya siasa ya ndani ya nchi



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akizungumza na Mwakilishi Mkazi mpya wa Shirika la Fedha Duniani (IMF) Bhaswar Mukhopadhyay Ikulujini Dar es Salaam.**

yaani kutetea maslahi ya nchi huko nje.

Kwa hivyo kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akiifanya ni kujenga na kuimarisha uongozi wa nchi kwa kuhimiza uwajibikaji na uongozi unaoleta matokeo. Katika hilo Rais amekuwa akichukua hatua mbalimbali kujenga taasisi za umma ili ziweze kuwa imara na zenye kuwajibika na ndizi zinazochangia kuiletea sifa Tanzania.

Mafanikio katika utekelezaji wa sera hizo za ndani ndiyo yanayoifanya Tanzania leo kung'ara katika medani za siasa za kimataifa. Taarifa za hivi karibuni kutoka New York kuwa Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Dk. Augustine Mahiga amekuwa na ratiba nzito kutokana na maombi ya midi kutoka kwa wajumbe wa nchi na taasisi malimbali za kimataifa inaonesha namna Rais Magufuli anavyokubalika.

Mwenye macho haambiwi tazama kwani yaliyotokea New York hayatofautiani na yale yanayotokea nyumbani ambapo wadau wa maendeleo zikiwemo nchi washirika, kila uchao, wamekuwa wakibisha hodi kuunga mkono hatua

zinazochukuliwa na uongozi wa Rais Magufuli katika kujenga Tanzania.

Washirika hao hawafichi maoni yao kuhusu utendaji wa Rais Magufuli na Serikali yake katika kuutengamanisha uchumi, kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji, hatua za kuimarisha ukusanyaji mapato na udhibiti wa matumizi ya Serikali, kukomesha vitendo vya rushwa na vita dhidi ya madawa ya kulevya pamoja na kuondoa urasimu katika serikali.

Tanzania kupeleka ujumbe mdogo kabisa wa watu wane kwenye mkutano huo, kama alivyonukuliwa Balozi Dk. Mahiga, ni tukio la kihistoria kwa kuwa hata katika kipindi ambacho taifa liliwahi kutangaza kuwa limo katika hali mbaya ya uchumi na wananchi kutakiwa kufunga mikanda haikuwa kusikika kuwa uwakilishi wa Tanzania katika mikutano ya kimataifa ulikuwa nawatunwachache kwa kiasi hiki. Kupunguza matumizi katika safari za nje ni moja katika ahadi ambayo Rais Magufuli amekuwa akiitekeleza kwa umakini mkubwa na kwamba sio tu imemjengea sifa yeye binafsi bali Tanzania yote na ndio maana

washirika wa maendeleo wamekuwa 'rahimu' kwa Tanzania. Alifanya hivyo kwa mkutano wa Jumuiya ya Madola uliofanyika mapema mwaka huu huko Malta ambapo Tanzania iliwakilishwa na Balozi wake nchini Uingereza.

Wakati akiwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki aliahidi kubana matumizi ambapo katika kipindi cha uongozi wake na kufanikiwa kuokoa Dola za Kimarekani milioni 2.5. Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake Mheshimiwa Rais amewaalika na kuitikiwa vyema na viongozi wa nchi mbali mbali zikiwemo Afrika Kusini, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC), Ethiopia, India, Misri, Morocco, Sudan Kusini, Uganda, Uturuki, Vietnam na Zambia.

Katika ziara hizo Tanzania imeweza kupigia chapuo malengo yake ya kidiplomasia, kiuchumi na kijamii na kufanikiwa kutiwa saini makubaliano mbali mbali ya ushirikiano yakiwemo ya kiuchumi hususan uwekezaji na biashara kuititia sekta binafsi. Aidha katika kipindi hicho, amewapokea wageni mashuhuri kutoka mashirika makubwa ya fedha ulimwenguni ikiwemo Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Mashirika hayo yote pamoja na kuridhishwa na utendajiwa uongoziwa Awamu ya Tano lakini pia yameahidi kuendelea kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo. Wakati akielekea kutimiza miaka miwili ya kwanza ya uongozi wake,

Rais Magufuli ameonesha umahiri mkubwa katika kuongoza siasa ya mambo ya nje ya nchi na kuonesha mfano wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Aidha, hadi sasa Rais Magufuli ameweza kuimarisha taswira ya Tanzania katika sura ya dunia na vile vile kuiwezesha Tanzania kuendelea na sifa yake ya kuwa nchi yenye ushawishi mkubwa katika siasa za kimataifa.

Kama somo la diplomasia linavyooleza kuwa Rais ndie mwanadiplomasia namba moja wa nchi na kioo cha nchi katika macho ya dunia, Rais Magufuli amedhihirisha kuwa kwa yeye ndie mwanadiplomasia namba moja wa Tanzania!

# Tanzania Yaonesha Mafanikio Katika Kutokomeza Malaria

**Na. Thobias Robert - MAELEZO**

Katika kipindi cha miaka miaka 15 kuitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP), Tanzania imekuwa ikipambana na ugonjwa wa malaria na vifo vinavyotokana na ugonjwa huo kwa lengo la kutokomeza kabisa kabisa ugonjwa huo ambao umekuwa ukisababisha vifo vingi hasa vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Katika kipindi hicho, NMCP kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo na wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi, wamebuni mikakati mbalimbali na kuitekeleza. Mikakati hiyo ni pamoja na kupulizia dawa yenye viuatilifu katika makazi ya watu, kutunza mazingira ya maeneo ya makazi, kupulizia viuatilifu katika maji yaliyotuama na kugawa vyandarua vyenye viuatilifu dhidi ya mbu waenezao malaria kote nchini.

"Kwa kipindi cha mwaka 2011 hadi 2015 maambukizi na vifo vinavyosababishwa na malaria vimepungua na ugonjwa huo haukuwa ugonjwa unaongoza kwa idadi kubwa ya watu waliopoteza maisha tofauti na iliyokuwa mwaka 2006 hadi 2010 ambapo ugonjwa huo ulikuwa unaongoza kwa idadi ya vifo vya watu wengi hapa nchini," anaeleza Dkt. Sigsbert Mkude, Kiongozi wa Uchunguzi na Matibabu kutoka NMCP.

Takwimu zinaonesha maambukizi ya malaria katika



**Makamu wa Rais wa Cuba Mhe. Salvador Valdez Mesa (kushoto) na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu wakimsilkiza Meneja Teknolojia wa Kiwanda cha Biotech Product kinachozalisha Viuadudu cha kuua Viluwiliwi vya Mbu vinavyoambukiza Malaria Bi. Lourdes Gonzalez, walipotembelea kiwanda hicho Mkoani Pwani**

mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Kagera, Mara, Shinyanga pamoja na mkoa wa Kigoma yalipungua kutoka asilimia 39 mwaka 2008 hadi asilimia 25 mwaka 2012 huku katika mkoa wa Lindi ikishuka kwa asilimia 27 wakati maambukizi yakiwa chini ya asilimia 0.5 kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini pamoja na Kanda ya Kati.

Katika vituo vya tiba, mwenendo unaonesha kuwa wagonjwa wa malaria nao wanapungua. Kwa mujibu wa Dkt. Mkude, halihyo imetokana na maboresho makubwa ya upimaji wa malaria katika vituo vya afya vya umma kwa asilimia 86 na kwamba upatikanaji wa dawa

na vitendanishi vya malaria umefikia kiwango cha asilimia 95. Moja ya mkakati muhimu wa Mpango wa NMCP ni kampeni ya utoaji wa vyandarua kwa wananchi hasa wajawazito na watoto. Hata hivyo bado wanakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo matumizi yasiyo sahihi ya vyandarua hivyo.

NMCP imeendelea kuweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuendelea kupunguza maambukizi ya malaria. Mingoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na usambazaji wa vyandarua kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja (Chandaria Kliniki) kwa



**Mtaalam wa Maabara ya Uandaaji Bakteria katika Kiwanda cha kuzalisha Viuadudu vya kuua viluwiluvi vya mbu wa malaria kilichopo Kibaha Mkoani Pwani, Bw. Fumbuka Pauline akiwaeleza waandishi wa habari (hawapo pichani) baadhi ya kazi wazifanyazo wakati wa kuwaandaa viuadudu vya kuua malaria 15 Mei, 2017.**

mikoa yote 26 ikiwa ni zoezi endelevu ambalo hufanyika pale mama anapohudhuria kliniki kwa mara ya kwanza na pia mtoto hupatiwa chandarau kila anapotimiza miezi tisa.

Mradi huu, hufadhiliwa na Mpango wa Rais wa Marekani wa Kudhibiti Malaria (USPMI) na hufanyika katika zahanati na hospitali zote za umma pamoja na zenye usajili wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Aidha, imeelezwa kuwa NMCP ina mpango wa kupulizia viuatilifu aina ya acctellc300CS katika halmashauri za Ngara, Bukoba na Misenyi mkoani, halmashauri za Ksimba, Sengerema na Buchosa mkoani Mwanza, Manispaa ya Musoma na Halmashauri ya Butiama mkoani Maranamkoawa Geita katika wilaya za Chato na

Nyangwale. Chini ya mpango huo kaya 574,000 na wananchi zaidi ya milioni 2.8 watanufaika. Mwezi Oktoba mwaka huu, NMCP inatarajia kusambaza zaidi ya vyandarua milioni 2.3 kwa mikoa 14 kupitia wanafunzi mashulenii. Mikoa hiyo ni pamoja na Morogoro, Mtwara, Ruvuma, Kagera, Geita, Mara, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Kigoma, Tabora, Katavi, na Pwani. Mpango wa ugawaji vyandarua ni sehemu ya ufadhili wa Mfuko wa USPMI.

Kampeni ya usambazaji vyandarua nchi nzima hufanyika kila baada ya miaka mitatu na itafanyika tena mwaka 2019 ambapo zaidi ya vyandarua milioni 15.4 vinatarajiwa kugawiwa kwa wananchi wa mikoa 12 ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Manyara,

Mbeya, Njombe, Rukwa, Singida, Songwe na Tanga.

Katika kampeni hiyo Mkoa wa Dar es Salaam unatarajia kupata vyandarua 3,916,697. Kampeni hii imekuwa ikifadhiliwa kwa pamoja na mfuko wa Kimataifa wa Kupambana dhidi ya UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu (Global Fund) pamoja na USPMI.

Mbali na mafanikio hayo, bado kuna changamoto katika suala la matumizi ya vyandarua ambapo baadhi ya wananchi wanavitumia kinyume na malengo ya mradi. Kwa mfano vyandarua kutumika katika uvuvi, katika ufugaji kuku na kufanywa uazio kwenye bustani pamoja na kugubikwa na imani potofu kuwa matumizi ya vyandarua hivyo hupunguza nguvu za kieme.

Tanzania inaweza kujifunza kutoka Zanzibar ambapo mwaka 1969 ilitokomeza kabisa ugonjwa huo. Sri Lanka katika miaka ya 1946 na 1960 nayo ilifanikiwa kuutokomeza ugonjwa huo lakini kutokana na kukosa umakini katika kuendeleza hatua za kudhibiti ugonjwa huo ulirejea tena.

Katika ziara yake ya hivi karibuni katika mkoa wa pwani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli alizitaka halmashauri mbalimbali nchini kutumia viuatilifu vinavyozalishwa na kiwanda cha Kibaha Biotech Products ili kunyonyizia katika maeneo ya halmashauri hizo kwa lengo la kutokomeza vimelea vya mbu wanaosababisha malaria.

# Mfumo wa Uagizaji Mbolea kwa Pamoja Kumkomboa Mkulima

**Na. Frank Shija -MAELEZO**

Tanzania ni moja kati ya nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara zenyenye matumizi ya chini sana ya mbolea.

Kwa sasa matumizi ya mbolea yamefikia wastani wa kilo 19 za virutubisho kwa hekta moja. Hii ni sawa na asilimia 38 ya azimio la Maputo lilioweka lengo la matumizi ya mbolea kufikia angalau kilo 50 za virutubisho kwa hekta moja.

Kufuatia hali hiyo Serikali imeweka mkakati utakao saidia kuhakikisha kunakuwepo kwa ongezeko la matumizi ya mbolea kwa wakulima hasa mbolea za kupandia na kukuzia mazao ili hatimaye kuinua sekta ya Kilimo kwa ujumla.

Kupitia taarifa yake kwa vyombo vyta ya Habari mwanzoni mwa mwezi wa tisa mwaka huu, Waziri wa Kilimo, Chakula na Mifugo Dkt. Charles Tizeba anasema kuwa kutokana na hali halisi ya matumizi madogo ya mbolea, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea Tanzania (TFRA) umefanya maboresho ya namna ya uagizwaji wa mbolea nchini ili kupunguza gharama hivyo utakuwa ukifanyika kwa pamoja chini ya uratibu wa Mamlaka hiyo.

"Kwa mujibu wa ibara ya 56 ya Kanuni za Mbolea (2011) na marekebisho yake ya mwaka 2017(The Fertilizer (Amendment) Regulations, 2017) na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali (GN) Na. 50 la



***Wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari nchini wakiendelea na zoezi la upakiasi wa mbolea ya kupandia tani elfu 23 tayari kwenda kwa wakulima baada ya kuingiza nchini hivi karibuni.***

Februari 17, 2017, mbolea aina zote zinatakiwa kuuzwa kwa bei iliyopangwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) iliyo chini ya Wizara ya Kilimo Mifugona Uvuvi," anasema Dkt. Tizeba kupita taarifa hiyo.

Mbolea zinazotumika hapa Tanzania kwa sasa ni pamoja na Minjingu, TSP, DAP, Urea, NPK, CAN na SA. Aidha, mbolea zingine zinazotumika ni zile za asili kama mboji na samadi. Kwa kuanzia, leo tunatatoa bei elekezi kwa mbolea za kupandia (DAP) na ya kukuzia (Urea). Bei elekezi kwa mbolea zingine zitatangazwa baadaye. Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea Tanzania (TFRA) Bw. Lazaro Kitandu anasema huduma ya upatikanaji wa mbolea kwa wakulima wote nchini utarahisishwa kwa

kuwa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Mifugo imeweka utaratibu mpya wa uagizaji wa mbolea kwa kutoa tenda kwa wazabuni mbalimbali.

"Serikali imechukua hatua ya kuanzisha utaratbu mpya wa kuagiza mbolea kwa pamoja kutoka zinakotengenezwa, yaani mbolea za kupandia (DAP) na mbolea za kukuzia (UREA) kupitia kwa wawekezaji wanaochukua zabuni hiyo," anasema Kitandu. Aidha Bw. Kitandu anabainisha kuwa taratibu za uagizwaji wa mbolea umekwisha kamiliika kwa kuwapata wazabuni, ambapo mbolea inatarajiwa kuwasili nchini mapema mwezi Septemba mwaka huu anaongeza kuwa itakuwa inaingizwa kwa awamu ya kila baada ya miezi miwili.

Anawataja


wazabuni

walioshinda tenda ya kuingiza mbolea nchini kuwa ni kampuni ya OCP ya Morocco na Premium Agrocam ya Tanzania amba moja itaingiza mbolea ya kupandia (DAP) na nyingine ya kukuzia (UREA).

Bw. Kitandu alivitaja vigezo vilivyotumika kumpata mzabuni huyo kuwa ni pamoja na bei inayopatikana katika viwanda vinavyotengeneza mbolea ambapo OCP pamoja na premium agrocam walionekana kuwa na bei za kuridhisha.

Aidha Bw. Kitandu anawahakikisha wakulima kuwa mbolea hiyo itakapowasili nchini itasafirishwa mpaka vijiji kwa kutumia treni na malori kwa sehemu ambapo treni haiwezi kufika, na anawatoa hofu wakulima kuwa msimu unaoanza mwezi wa tisa wameagiza tani 23,000 kwa mbolea ya kupandia (DAP) na tani 32,000 kwa mbolea ya kukuzia (UREA) ambapo watakuwa wanaagiza kwa awamu kwa miezi miwili miwili.

"Tanzania inatumia Tani milioni nne kwa mwaka na kwa msimu huu bei ya mbolea itashuka



**Wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari nchini wakiendelea na zoezi la kufunga mbolea ya kupandia katika mifuko tayari kwa kupakiwa na kusafirishwa kwenda kwa wakulima.**

kutoka asilimia 15 mpaka asilimia 40, ambapo kwa mfuko wa kilo 50 utanunuliwa kwa shilingi 52,000 badala ya shilingi 100,000 bei ya awali". anasema Kitandu.

Ndoto ya nchi yetu ni kuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda ifikapo mwaka 2025, uchumi ambao huhitaji mali ghafi nyingi zitokanazo na

mazao ya kilimo. Kwa kutambua hilo Serikali ya Awamu ya Tano imekuja na mkakati huu wa kuwa na bei elekezi na mfumo wa uagizaji wa pamoja ili kuhakikisha mkulima mdogo analima kwa tija kwa njia ya kuongeza matumizi ya mbolea na ni mategemeo kuwa mfumo huu mpya utatoa ahueni kwa mkulima jambo litakalomfanya amudu gharama.

## TACAIDS: Ukimwi Bado ni Changamoto

**Na. Fatma Salum -MAELEZO**

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) immeendelea kuiasa jamii kuhusu kubadili tabia ili kuepuka maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwani ugonjwa huo bado ni janga kwenye nchi yetu.

Hayo yamesemwa mwishoni

mwa wiki Jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa tume hiyo Bw.Jumanne Issango alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio na changamoto za tume tangu ilipoanza kutekeleza majukumu yake.

"UKIMWI bado ni changamoto katika maendeleo ya Taifa letu na umeendelea kuathiri kila sekta, kila imani, matajiri

na masikini nchini kote hivyo ni wajibu wa kila mmoja kujitathmini mwenendo wake na kuacha tabia hatarishi ambazo zinachangia kuongeza maambukizi ikiwemo uasherati, ngono zembe, ulevi na kadhalika," alisema Bw.Issango.

Alieleza kuwa kwa miaka ya hivi karibuni hali ya maambukizi ya UKIMWI



**Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TACAIDS Bw.Jumanne Issango akieleza jambo kwa waandishi wa habari (hawapo pichani) wakati akitoa tathmini kuhusu changamoto na mafanikio katika kupambana na virusi vya ukimwi nchini, kulia ni Kaimu Mkurugenzi Muitiko wa kitaifa wa TACAIDS Bi. Audrey Njelekela**

imeendelea kupungua ingawa kuna tofauti kwenye mikoa, wilaya na makundi ya kijamii.

Bw.Issango alibainisha kuwa kiwango cha maambukizi Tanzania Bara ni asilimia 5.3 na takwimu hizo ni kutokana na utafiti wa viashiria vya UKIMWI wa mwaka 2012.

Kwa mujibu wa utafiti huo Wanawake walioambukizwa ni asilimia 6.2 na Wanaume ni asilimia 3.8 ambapo idadi ya Watanzania wanaokadiriwa kuishi na VVU nizaidi ya milioni 1.5.

"Mikoa inayoongoza kuwa na maambukizi makubwa ni Njombe asilimia 14.8, Mbeya asilimia 9 na mikoa yenye maambukizi ya chini zaidi ni Manyara asilimia 1.5, Tanga asilimia 2.4 na Dodoma asilimia 2.9," alifafanua Bw.Issango.

Aidha alisema kuwa licha

ya maambukizi mapya kupungua kwenye jamii bado kiwango cha maambukizi kwenye makundi maalum kimeendelea kuongezeka.

Makundi ambayo kiwango cha maambukizi kimeongezeka ni pamoja na madereva wa magari ya masafa marefu, wachimba madini, wavuvi, wafungwa na wale wanaofanya biashara yangono.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Idara ya Muitiko wa Kitaifa kutoka Tume hiyo Bi. Audrey Njelekela alisema Serikali kuitia TACAIDS inaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na janga hilo ikiwemo kuandaa na kutekeleza mikakati madhubuti itakayosaidia kupunguza maambukizi kwa kiasi kikubwa.

"Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI 2013/14

- 2017/18 unalenga ifikapo 2018 kiwango cha maambukizi kishuke kufikia asilimia 0.16 ikilinganishwa na mwaka 2012 ambapo utafiti unaonesha maambukizi ni asilimia 0.32," alisema Bi.Njelekela.

Hatua nyingine zinazochukuliwa na tume hiyo ili kudhibiti maambukizi ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma hasa kwa vijana, wanawake wajawazito na makundi maalum ikiwemo kujenga Vituo vya Maarifa vinavyotoa huduma za VVU/UKIMWI kwa madereva wa magari ya masafa marefu.

Aliongeza kuwajuhudu za Serikali kutoa dawa za kufubaza makali ya Virusi vya UKIMWI (ARVs) zimesaidia kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo ambapo kwa sasa wanaotumia dawa hizo ni zaidi ya watu laki 8.

Pia Serikali imeanzisha Mfuko wa Udhagini wa Shughuli za Kudhibiti UKIMWI kwa ajili ya kusaidia kununua dawa, kutoa elimu ya UKIMWI, kupima, kufanya tafiti na kutoa elimu ya uzazi kwa vijana.

TACAIDS ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 22 ya mwaka 2001 kwa lengo la kutoa uongozi wa kimkakati, uratibu na kuimarisha juhudzi za wadau wote wanaojishughulisha


**"Serikali imeendelea kutoa dawa za kufubaza makali ya Virusi vya UKIMWI (ARVs) ambazo zimesaidia kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo, kwa sasa wanaotumia dawa hizo ni zaidi ya watu laki 8" alisema Bw. Issango**

# KATUNI NA MSAMIATI WA LEO



## KUTOKA KAMUSIKUU YAKISWAHLI TASHTITI

*Kitendo cha Mtu kumkera mtu mwingine kwa kurudia jambo lilelile au kwa kumlazimisha mtu vis.: chagizo, kero B. (fasih) Usemi unaosemwa kwa lengo la kumkejeli mtu k.m. ‘amepaka mafuta mazuri mpaka nzi wanamfuata kila aendako’*



# TANZANIA SEPTEMBA



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. John Pombe Magufuli akikagua gwaride ya maafisa wapya kundi la 61/16 kabla ya kuwatunuku kamisheni kuwa maafisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha Septemba 23, 2017.**



**Meja Jenerali Michael Isamuhyo akitembelea na kuoneshwa eneo la vitalu A mpaka D katika eneo la machimbo ya madini ya Tanzanite Mererani wilaya ya Simanjiro Mkoani Manyara Septemba 21, 2017, tayari kwa kuanza kazi ya kujenga uzio kuzunguka eneo hilo kufuatia amri ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli.**



**Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa akifurahia baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Longido mkoani Arusha Septemba 21, 2017. Wa pili kushoto ni Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mhandisi Gerson Lwenge na kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mrisho Gambo. Kulia ni Mbunge wa Hanang Dkt. Mary Nagu.**



**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Bi. Ineke Bussemaker ambaye alifika Ofisini kwa Makamu wa Rais, Ikulu jijini kumtembelea Dar es Salaam**

# NCHII YETU KATIKA HISTORIA




*Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (katikati) akishiriki katika uzinduzi wa mbio za magari za East Afrika Safari Machi 30, 1972*



*Mabalozi wa Tanzania waliopo nchi za nje wakitembelea kijiji cha Ujamaa cha Kawawa Mkoani Mtwara ili kuona makazi mapya ya wananchi, Machi 17, 1969*



*Hayati Waziri Mkuu Edward Moringe Sokoine akiongea na wakazi wa kijiji cha Ujamaa na Ulinzi cha Mazinguri Wilaya ya Masasi ambapo aliwaomba kuwa makini na hila za mabepari, Septemba 13, 1971*



*Wanakijiji cha Ujamaa cha Lulanzi, Iringa wakiwa kiwandani wakitengeneza Makoroboi na Ndoo*

# Tanzania Yawa “Donor Country” Tiba ya Moyo

**Na. Judith Mhina-MAELEZO**

Katika miaka ya hivi kkaribuni mataifa mengi yanayoendelea yamekuwa yakifanya mabadiliko makubwa katika mfumo wa huduma ya afya ili kuendana na viwango vya kimataifa vilivyowekwa na nchi za Ulaya na Marekani.

Tanzania ni Kati ya nchi zinazoendelea ambazo zimepiga hatua katika kutatua changamoto mbalimbali za matibabu Afrika Mashariki na kufanikiwa zaidi katika masuala ya matibabu ya moyo ambapo wagonjwa 21 kutoka nje ya nchi wamepata huduma ya operesheni na kuzibua mishipa ya moyo, katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Akitoa taarifa hiyo Afisa Mawasiliano wa JKCI Bw. Maulid Mohammed amesema wagonjwa hao ni kutoka mataifa ya Kenya (1) Uganda (1) Rwanda (2) Malawi (2) Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (5) Komoro (10).

Kutokana na huduma hiyo ya upasuaji na uzibuaiji wa mishipa ya moyo hapa nchini, Serikali imeokoa fedha nyingi.

Mfano mwaka 2015 operesheni ishirini zilizofanyika kwa watanzania ziliokoa fedha za Tanzania Shilingi milioni 340 na kutumika milioni 160 tu. Kama wagonjwa hao wangesafirishwa nje ya nchi wangehitaji fedha za Tanzania milioni 500, ambapo gharama kwa mtu mmoja nje ya nchi ni milioni 25 lakini kwa JKCI hapa Tanzania ni milioni nane.

Aidha, idadi kubwa ya



**Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Ummy Mwalimu (katikati) akikata utepe wakati wa hafla ya makabidhiano ya vifaa tiba kwa ajili ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete hivi karibuni jijini Dar es Salaam, kulia ni Balozi wa Kuwait nchini Tanzania Jasen Al Najem na kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo Prof. Mohamed Janabi.**

wagojwa kutoka nje ya nchi, ni wale wanaopata matibabu na kuondoka(OPD)ambaponchiya Comoro imekuwa kuwa na zaidi ya wagonjwa 100 kwa mwezi.

Hata hivyo viongozi mbalimbali kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wanatembelea hospitali hii kwa lengo la kutaka kuanzisha katika nchi zao.

Bw. Mohammed amesema ongezeko la wagonjwa kuja Tanzania kwa ajili ya matibabu limehamasisha Serikali kuendelea kuboresha hospitali mbalimbali hapa nchini hasa katika eneo la vifaatiba na utaalamu.

Hivyo, imekuwa ni rahisi kwa wataalamu mbalimbali duniani kuja kushirikiana na madaktari wazawa katika kutoa matibabu sahihi kwa wagonjwa na kuoko mamilioni

ya fedha ambayo, yalikuwa yanalipwa ili kuokoa maisha ya watanzania walitaabika kwa maradhi ya moyo.

Aidha, Serikali ilikuwa ikitumia fedha za Tanzania bilioni 2.5 kwa mwaka kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa wa magonjwa mbalimbali nje ya nchi, ambapo idadi kubwa walikuwa ni wagonjwa wa Moyo.

Mabadiliko katika ubora wa huduma ya matibabu yamekuwa na matokeo makubwa katika sekta ya utalii wa kimatibabu. Moja ya nchi zilizo mbele katika mabadiliko ni India ambayo inachangiwa na ukuaji mkubwa wa uchumi katika miaka ishirini iliyopita.

India inatambulika kama moja ya nchi inayopokea watu wengi duniani kwa ajili



**Wataalamu wa Magonjwa ya Moyo wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) na wataalam Kutoka Taasisi ya Madaktari Afrika ya Nchini Marekani wakimwekeea mgonjwa kifaa maalum cha kurekebisha mapigo ya moyo.**

ya matibabu ya kina zaidi.

Kama taifa linaloendelea gharama zinazotakiwa kwa ajili ya matibabu ni nafuu kulinganisha na mataifa yaliyoendelea. Hii inawezeshwa na ukuaji wa miundombinu na vifaa pamoja na teknolojia ya hali ya juu inayo ifanya India iwe sambamba na maendeleo yaliyopo Marekani au Ulaya.

Tanzania kama Taifa linaloendelea tunapaswa kuunga mkono juhudhi zote zinazofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwekeza katika kuinua viwango vya hospitali zetu kama ujenzi mbalimbali unaofanywa na Taasisi ya Benjamin Mkapa. Pamoja na hayo, ni muhimu kuwa na utaalamu na weledi wa hali ya juu ili kuwawutia wagonjwa kija nchini kwako, ambapo serikali imejenga hospitali ya Mronganzira ikiwa maaluum kwaajiliyaMadaktariwanafunzi.

### UTALII WA KIMATIBABU NCHINI INDIA

Huduma bora na za kisasa za matibabu zinazotolewa na nchi zilizoendelea katika sekta ya afyazimesababishawatukota mataifa mbalimbali kwenda kufuata huduma hizo nje ya mataifa yao na kuunda sekta ya aina yake ijlukanayo kama utalii wa kimatibabu (medical tourism) ambapo watu kutoka mataifa mengine husafiri kwenda nchi nyingine kupata matibabu.



**Dr Med Henning Niebuhr kutoka Ujerumania kitoa maelekezo juu ya namna ya kufanya upasuaji kwa njia ya vitundu**

Moja ya nchi zinazopokea wagonjwa wengi ni India.

Inakadiriwa kuwa mgonjwa kusafiri kwenda India kwa sababu za matibabu unaweza kuokoa asilimia 70 hadi 75 ya jumla ya gharama bila kujali anakwenda kwa ajili ya aina gani ya matibabu. Chama cha madaktari wa Marekani (American Medical Association) hivi karibuni kilifanya utafiti juu ya gharama zinazotakiwa kwa ajili ya upasuaji mbalimbali na matokeo kuonyesha kuwa India ina gharama ndogo za matibabu, mara tatu chini ukilinganisha na nchi za magharibi na bado ni kiasi kidogo ukilinganisha na mataifa mengine ya Asia.

Kuchukua mfano wa upasuajiwa goti katika maeneo mbalimbali, wastani wa gharama ni dola 40,000 katika hospitali za Marekani, dola 10,000 katika hospitali za Thailand lakini India gharama ni dola 8,500.

## ZIARA YA RAIS MAGUFULI MIKOA YA ARUSHA NA MANYARA



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Profesa Makame Mbarawa (kulia) wakizindua rasmi barabara ya lami ya kilomita 26 kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) katika mkoa wa Kilimanjaro hadi Mererani mkoani Manyara Septemba 20, 2017.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli akiwa pamoja na viongozi wengine wakikata utepe kuzindua barabara ya lami ya kilomita 26 kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) katika mkoa wa Kilimanjaro hadi Mererani mkoani Manyara Septemba 20, 2017.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akizungumza na wananchi wa njiapanda ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea mkoa wa Arusha alipokuwa na ziara ya siku 6 kuanzia septemba 20, 2017 hadi Septemba 25, 2017.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akiwa na Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro Bi. Anna Mgwila (kushoto) na Mkuu wa mkoa wa Arusha Bw. Mrisho Gambo(kulia) katika uwanja wa ndege wa kimataifa KIA alipomaliza ziara ya kikazi ya siku 6 kwenye Mikoa ya Arusha na Manyara kuanzia septemba 20, 2017 hadi Septemba 25, 2017.*



## MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA NI KIMBILIO LA WASTAAFU KWA AFYA BORA

Mwanachama Mstaafu wa NHIF atanufaika na:-

- Huduma za matibabu yeye na mwenza wake maisha yao yote bila kuendelea kuchangia.
- Watanufaika na mafao yote yanayotolewa na NHIF.

Mwanachama mara unapostaafu zingatia yafuatayo:-

- Kuwasilisha barua ya kustaafu.
- Kurejesha kitambulisho chako cha matibabu na vya wategemezi wako.

PATA HUDUMA ZA MATIBABU KWA KADI YA NHIF POPOTE NCHINI KATIKA VITUO ZAIDI YA 6000 VIVIVYOSAJILIWA NA NHIF

\* kwa maelezo zaidi wasiliana na NHIF huduma kwa wateja 0800 110063

[www.nhif.or.tz](http://www.nhif.or.tz) | [info@nhif.or.tz](mailto:info@nhif.or.tz) | 0800 110063



Welcome to Generation T.Solved

LIMEANDALIWA NA

*Idara ya Habari-MAELEZO*

*S.L.P 8031*

*Dar es Salaam-Tanzania*

*Simu : (+255) 22 -2122771*

*Barua pepe:maelezo@habari.go.tz*

*Tovuti: www.maelezo.go.tz*

*Blogu: blog.maelezo.go.tz*

